

Safari ya Mwisho ya Mwokozi, Safari ya Upweke

Na Chakell Wardleigh
Magazeti ya Kanisa

Katika maisha Yake yote ya duniani, Mwokozi alipitia safari nyingi—safari Yake kutoka Bethlehemi na kwenda Misri akiwa mtoto mchanga, safari Yake ya siku-40 nyikani, safari Zake nyingi mijini, vijijini, na majumbani kufundisha, kuponya, na kubariki wakati wa huduma Yake, na nyingine nyingi. Lakini kuna safari moja ambayo Mwokozi alipaswa kuipitia peke yake, na ilikuwa safari ambayo ni Yeye pekee ndiye angeweza kuivumilia.

ECCE HOMO, NA LOUIS ROYER, RIJKSMUSEUM

“Katika Jumapili ya Pasaka tunasherehekea tukio kuu na tukufu lililosubiriwa zaidi katika historia ya ulimwengu.

“Ni siku ambayo ilibadilisha kila kitu.

“Katika siku hiyo, maisha yangu yalibadilika.

“Maisha yako yalibadilika.

“Hatima ya watoto wote wa Mungu ilibadilika.”

Rais Dieter F. Uchtdorf, Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, “Zawadi ya Neema,” *Liahona*, Nov. 2015, 107.



Simon Dewey

EE BABA YANGU, NA SIMON DEWEY

Kuteseka kusio na Kifani

Hakuna akili ya kidunia inayoweza kupokea maana yote ya kile ambacho Kristo alifanya katika Gethsemane.

“Tunajua alitoka jasho jingi la damu kwenye kila kinyweleo alipokuwa akinywa mashapo ya kile kikombe kichungu ambacho Baba yake alimpa.

“Tunajua aliteseka, vyote viwili mwili na roho, zaidi ya inavyowezekana mwanadamu kuteseka, isipokuwa tu katika kifo.

“Tunajua kwamba katika njia fulani, zisizoeleweka kwetu, mateso yake yaliridhisha madai ya haki, akikomboa nafsi zenye kutubu kutokana na maumivu na adhabu ya dhambi, na kufanya rehema ipatikane kwa wale waaminio katika jina lake takatifu.

“Tunajua kwamba aliaanguka kifudifudi juu ya ardhi wakati maumivu na mateso ya mzigo usio na mwisho yalimsababisha atetemeke na kutamani kwamba asinywe kikombe kile kichungu.”

Mzee Bruce R. McConkie (1915–85) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, “The Purifying Power of Gethsemane”, *Ensign*, Mei 1985, 9.

Matumizi Binafsi: Japokuwa tunaweza daima tusitambue, Huyu Mwokozi aliteseka aina zote za maumivu wakati wa Upatanisho. Yeye anaelewa kila maumivu ya kimwili, kuanzia mfupa uliovinjika mpaka kwenye ugonjwa wa muda mrefu wenye maumivu makali. Alihisi giza na kukata tamaa kwa maradhi ya akili kama vile mfaadhaiko, wasiwasi, uraibu, upweke, na huzuni. Na alilisia kila jeraha la kiroho kwa sababu alijichukulia juu Yake dhambi zote za wanadamu.

Mzee David A. Bednar wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili alifundisha, “Katika wakati wa udhaifu tunaweza kulia, ‘Hakuna anayejua jinsi ilivyo. Hakuna anayeelewa.’ Lakini Mwana wa Mungu anajua vizuri kabisa na anaelewa, kwani aliona na kubeba mizigo yetu ya kibinafsi” (“Walibeba Mizigo Yao kwa Urahisi,” *Liahona*, Mei 2014, 90).